TANGAZO LA SERIKALI NA. 459 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya wilaya ya hai ya Mwaka 2024.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa pale muktadha utahitaji vinginevyo:

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Bajaji" maana yake ni chombo cha usafiri chenye matairi matatu.

"Chombo cha Usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha mtu, watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa Baiskeli, Mkokoteni, au wanyama wanaotumika kusafirisha watu au mizigo;

"Halmashauri"maana yake ni Halmashauri ya wilaya ya Hai;

Sura ya 212

"kampuni" maana yake ni kama ilivyofafanuliwa chini ya Sheria ya kampuni;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi

inayotolewa na Halmashauri;

"kituo cha Mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kushusha abiria na mizigo ya Abiria;

"kodi ya Huduma" maana yake ni ada au ushuru inayotozwa na Halmashauri kutoka kwa kampuni au taasisi zinazofanya biashara au kutoa huduma katika Halmashauri;

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi za wanyama waliochinjwa;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"maegesho'' Sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha chombo cha usafiri kwa muda;

"makazi" maana yake ni jengo lolote linalo tumiwa kwa kuishi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Hai au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha shughuli za kuuza na kununua bidhaa;

"mnyama" maana yake ni mbuzi, ng`ombe, nguruwe na wanyama wengine wowote wanaofugwa na binadamu;

"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa matumizi ya soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"teksi" maana yake ni gari linalotumika kubeba abiria wasiozidi wanne;

"usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya mamlaka ya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa

na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"wakala" maana yake ni mtu binafsi,kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa Ada au Ushuru

**4**.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(5) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika;-

(6) Huduma zitakazotozwa ada au ushuru katika sharia ndogo hii ni;

(a) ada ya kukodi mali za halmashauri; ambapo baadhi ya mali zitatozwa kulingana na makubaliano yatakayoingiwa kwenye mkataba, kama vile magari, mitambo, vibanda, viti, mashamba ya halmashauri, ukumbi, treka na mali nyingine;
(b) ushuru wa madini ya ujenzi;
(c) ada na ushuru wa soko;
(d) ushuru wa mifugo;
(e) ada ya kibali cha kusafirisha mifugo;
(f) mazao ya chakula yatatozwa 2%;
(g) mazao ya biashara yatatozwa 3% ya bei ya

kununulia;

(h) ada ya huduma za machinjio, ukaguzi wa nyama;

(i) ushuru wa mazao ya misitu;

(j) ada ya vibali ya ujenzi na ukarabati wa majengo, ambapo kibali kinatakiwa kudumu kwa miezi sita tu, baada ya miezi sita hakitahesabika kama ni kibali;

(k) ada ya zabuni za Halmashauri;

(l) ada ya maegesho;

(m) ada ya vibanda na Ushuru wa Stendi;

(n) ada ya mashamba ya ushirika;

(o) Na ada nyingine kama zilivyoainishwa kwenye Jedwali la kwanza;

(7) Bila kuathiri masharti ya kanuni hizi, Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalum kuruhusu shughuli za usafirishaji wa bidhaa yoyote kufanyika nje ya muda ulioainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

**5**. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

**6**.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa kwenye kanuni hii.

Ukusanyaji wa madeni

**7**.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni

la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika kanuni ndogo ya (3) na (4), Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

**8**.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

**9**. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia Saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi Saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au

kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kuanzisha Soko

**10**.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuanzisha soko mahali popote katika eneo la Halmashauri kama itakavyoona inafaa kwa kuzingatia mahitaji wa Wananchi na matakwa ya Sheria za Mipango Miji na kulitangaza.

Sura ya 355

(2) Katika michoro ya mipango miji na utekelezaji wake, Halmashauri itatenga maeneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa soko.

Muundo wa Soko

**11**.-(1) Halmashauri itagawanya soko katika vyumba, vibanda, vizimba na stoo kwa ajili ya kurahisisha matumizi bora ya Soko.

(2) Matumizi ya soko yatazingatia mpangilio wenye mahusiano ya bidhaa zitakazouzwa Sokoni

Upangaji

**12**.-(1) Halmashauri itapangisha chumba, kibanda, kizimba au stoo kwa wafanyabiashara kwa mujibu wa taratibu na viwango vya kodi ya pango vitakavyowekwa kwenye mkataba ya pango.

(2) Mfanyabiashara atakayehitaji kupanga eneo la soko atawasilisha maombi yake kwa Halmashauri na akikubaliwa ataingia mkataba utakaonyesha muda, kiwango cha kodi ya pango, wajibu na taratibu za kufuata katika kipindi chote cha mkataba alichokubaliwa kufanya biashara.

(3) Mkataba wa upangaji unaweza kusitishwa endapo:-

(a) muda wa upangaji utakapokwisha;

(b) upande mmoja wa mkataba kutoa taarifa ya maandishi ya siku thelasini kwa upande mwingine ukitoa kusudio la kusitisha mkataba;

(c) Mfanyabiashara atapoteza sifa kutokana na kukiuka taratibu za Sheria Ndogo hii

(4) Baada ya muda wa upangaji ndani ya Mkataba kumalizika, mkataba mpya utafanyika kwa njia ya zabuni au kwa namna ambayo Halmashauri itaona inafaa.

(5) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kufunga kibanda au kizimba chochote ambacho hakijalipiwa

ushuru kwa miezi miwili mfululizo.

Uteuzi wa Msimamizi wa Soko

**13**. Halmashauri itamteua afisa yeyote kuwa msimamizi wa soko ambaye kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatambulika kama afisa masoko.

Wajibu wa Afisa Masoko

**14**. Afisa masoko atakuwa na wajibu wa:-

(a) kusimamia shughuli za kila siku za uendeshaji wa masoko yaliyopo katika eneo la Halmashauri;

(b) kwa kushirikiana na wadau wengine wa afya, mapato na mazao anaweza kuzuia uuzaji wa mazao au bidhaa sokoni iwapo kwa maoni yao bidhaa au mazao hayo yanaweza kuleta madhara kwa watumiaji au kusababisha uchafu wa soko;

(c) kuandaa na kutunza orodha ya wafanyabiashara wa sokoni; na

(d) atashirikiana na uongozi wa soko katika kupanga, kutekeleza na kutatua changamoto za uendeshaji wa soko.

Kamati ya Soko

**15**.-(1) Kutakuwa na kamati ya soko itakayoundwa na wafanyabiashara na wadau wengine wa soko.

(2) ukubwa wa kamati ya soko utategemeana na wingi wa wafanyabiashara katika soko husika.

(3) Bila kuathirimasharti ya kanuni ndogo ya (1) uongozi wa soko utaunda na kugawa kamati ndogo ndogo nyingine za wadau wa soko kama ifuatavyo:

(a) Kamati Ndogo ya miundombinu na usafi

(b) Kamati Ndogo ya biashara na utawala; na

(c) Kamati ndogo ya Ulinzi na Usalama

(4) Kamati zilizoainishwa kwenye kanuni ndogo ya (3) zitakuwa na wajumbe wasiozidi wanne.

Kazi za Kamati ya Soko

**16**. Kazi za Kamati ya soko zitakuwa kama ifuatavyo-

(a) kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji wa biashara na utendaji wa soko ili kuinua ustawi wa soko.

(b) kuanzisha na kuhamasisha uundwaji na kujiunga katika vyama vya ushirika
(c) kudhibiti nidhamu, usafi na matumizi sahihi ya soko na vyoo vya sokoni; na
(d) kuratibu mipango ya kugharamia huduma za ulinzi, usafi, maji na umeme kwa kadri itavyopangwa

Saa za Soko

**17**.-(1) Muda wa kuanza shughuli za Soko utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni kila siku.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) hapo juu, Halmashauri inaweza kuruhusu shughuli za Soko baada ya muda ya muda ulioainishwa kwenye kanuni hii.

Tahadhari ya Moto

**18**. Mtu yeyote hataruhusiwi kupika chakula, kuchoma nyama au kuendesha shughuli za mgahawa au shughuli yoyote inayohusisha moto ndani ya eneo la soko isipokuwa katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili ya Shughuli hii

Milango kwa matumizi ya dharula

**19**. Halmashauri itatenga maeneo maalum katika soko kwa ajili ya kukusanyika endapo kutatokea dharura yoyote au kuweka milango maalumu kwa ajili ya matumizi kipindi cha dharura.

Upakuaji mizigo katika masoko

**20**.-(1) Mazao na bidhaa mbalimbali zitasafirishwa na kuingizwa sokoni kwa kutumia vyombo vya usafiri, kisha mizigo itapakuliwa na vyombo hivyo vitaondoka sokoni ndani ya masaa sita au kadiri itakavyoelekezwa na afisa wa soko.

(2) Halmashauri itatoza ushuru wa magari yote yatakayoingia katika eneo la soko, kwa ajili ya kununua bidhaa au kupakia na kupakua bidhaa.

Makosa

**21**. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:
(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa

au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii; au

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

Adhabu

**22**. Mtu atakayekiuka masharti ya Sheria hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

**23**. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

**JEDWALI LA KWANZA**

*(limetengenezwa chini ya kanuni ya 4 (1))*

**SEHEMU YA KWANZA**

**NYUMBA ZINAZOMILIKIWA NA HALMASHAURI**

| Namba | Aina ya chanzo | Kiwango cha ushuru(shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Daraja la kwanza | 50,000/= kwa mwezi |
| 2. | Daraja la pili | 35,000/= kwa mwezi |
| 3. | Daraja la tatu | 20,000/= kwa mwezi |
| 4. | Maombi ya kumiliki viwanja | 20,000/= kwa kila fomu |
| 5. | Banda la Ngozi | Kwa mujibu wa Mkataba |
| 6. | Jengo la Nanenane Arusha | Kwa mujibu wa Mkataba |
| 7. | Nyumba nyingine za Halmshauri ambazo hazikutajwa | Kwa mujibu wa Mkataba |

**SEHEMU YA PILI**

**USHURU WA YA UJENZI**

| Namba | Aina ya chanzo | Idadi | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Kokoto,mchanga,mawe, moramu,udongo na changarawe na madini mengine ya ujenzi yatakayopatikana | Sentimita moja hadi saba | 10,000/= |
| | | Sentimita 7 hadi kumi na nne | 15,000/= |
| | | Sentimita kumi nne na kuendelea | 20,000/= |

**SEHEMU YA TATU**

**ADA NA USHURU WA SOKO**

| Namba | aina ya ada au ushuru | Chanzo cha ada au ushuru | kiwango cha ada au ushuru |
|---|---|---|---|
| 1. | Kodi ya pango kwa kizimba | Gezaulole,Soko la Walaji Bomang'ombe na masoko mengine ambayo hayakutajwa hapa. | 300/= kwa siku |

**SEHEMU YA NNE**

**USHURU WA MINADA YA MIFUGO**

| Namba | Aina ya Mfugo | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa ng'ombe | 2,000/= kwa kila mmoja. |
| 2. | Ushuru wa nguruwe | 2,000/= kwa kila mmoja. |
| 3. | Ushuru wa mbuzi na kondoo | Robo kilo kwa bei ya soko |
| 4. | Kuku au kanga au bata | 2,000/= kwa tenga . |

**SEHEMU YA TANO**

**ADA YA KIBALI CHA KUSAFIRISHA MIFUGO**

| Namba | Aina ya mfugo | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,000/= kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 1,500/= kwa kila mmoja |
| 3. | Kondoo | 1,500/= kwa kila mmoja |
| 4. | Nguruwe | 1,000/= kwa kila mmoja |
| 5. | Kuku au bataa kanga | 100/= kwa kila mmoja |
| 6. | Wanyama Wengine ambao hajatajwa | 4,000/= kwa kila mmoja |

**SEHEMU YA SITA**

**ADA YA HUDUMA ZA MACHINJIO, UKAGUZI WA NYAMA NA USHURU WA BUCHA.**

| Namba | aina ya chanzo | kiwango cha ada au ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Kwa kilo kwa bei ya soko |
| 2. | Kondoo na mbuzi | Kwa robo kilo kwa bei ya soko |
| 3. | Nguruwe | Kwa kilo kwa bei ya soko |

**SEHEMU YA SABA**

**USHURU WA NGOZI**

| Namba | aina ya ngozi | kiwango cha ushuru (shilingi) | idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Ngozi ya Ng`ombe | 500/= | Kwa kila ng'ombe 1 |
| 2. | Ngozi ya Mbuzi | 500/= | Kwa kila mbuzi 1 |
| 3. | Ngozi ya Kondoo | 500/= | Kwa kila kondo 1 |

**SEHEMU YA NANE**

**USHURU WA MAZAO YA MISITU**

*Tangazo La Serikali Na. 459 (Linaendelea)*

| Namba | chanzo cha ushuru | kiwango cha ushuru (shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kuni za miti laini | 10,000/= kwa tani 1. |
| 2. | Mkaa Gunia moja | 2,000/= |
| 3. | Mbao- bila kujali unene mti laini | 200/= kwa ubao |
| 4. | Mbao- bila kujali unene mti asili | 1,000/= kwa ubao |
| 5. | Nguzo-bila kujali unene Mti laini | 300/= kwa nguzo |
| 6. | Nguzo-bila kujali unene Mti asili | 2000/= kwa nguzo fito |
| 7. | Mbao zinazosafirishwa nje ya Halmashauri | 300/= kwa kila gogo |
| 8. | Miti laini ya nguzo za umeme | 1000/= kwa gogo |
| 9. | Magogo ya kuni | 500/= kwa gogo |
| 10. | Asali Nyuki | |
| | (i)Nyuki wakubwa | 5% ya bei ya mauzo ya soko kwa kila lita |
| | (ii)Nyuki wadogo | 5% ya bei ya mauzo kwa kila lita |
| 11. | Magogo “mete” yanayotumika viwandani kwa ajili ya nishati ya moto | 10,000/= kwa tani1 |
| 12. | Magome ya Miti | 5,000/= kwa tani 1 |

## SEHEMU YA TISA

## ADA YA IDHINI YA UJENZI

| Namba | aina ya jingo | kiwango cha ada (shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba zote za Makazi, ghorofa na nyumba za biashara | 500/= kwa mita moja ya mraba |
| 2. | Ghala au Bohari | 400,000/= |
| 3. | Usimikaji wa minara ya Simu | 5,000,000/= |
| 4. | Vituo vya mafuta | 500,000/= |

## SEHEMU YA KUMI

## ADA YA MABADILIKO YA JENGO LILILOPO

| Namba | Aina ya jingo | Kiwango cha ada |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba ya makazi au biashara au ghorofa | 500/= kwa mita moja ya mraba |

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA

## ADA YA KUPIMIWA ARDHI

| Namba | Aina | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Kiwanja Kidogo | 80,000/= |
| 2. | Kiwanja cha Kati | 120,000/= |
| 3. | Kiwanja kikubwa | 150,000/= |

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI

## UZIO WA UKUTA WA KUDUMU

### A: MAENEO YA KUISHI

| **Namba** | **Aina ya ada** | **Kiwango cha ada** |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kibali | 150 /= Kwa kila mita ya urefu |
| 2. | Ada ya Ukaguzi wa ramani, Nyaraka na ujenzi | 100/= kwa mita |

### B: MAENEO YA BIASHARA

| **Namba** | **Aina ya ada** | **Kiwango cha ada** |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kibali | 200 /= Kwa kila mita ya urefu |
| 2. | Ada ya Ukaguzi wa ramani, Nyaraka na ujenzi | 120/= kwa kila meta ya urefu |

### C: UJENZI WA UZIO

| **Namba** | **Aina ya ada** | **Kiwango cha ada** |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kuweka uzio wakati wa ujenzi kwa muda usio zidi Mwezi mmoja | 100/= kwa kila mita ya urefu |
| 2. | Ada ya kuwek a uzio wakati wa ujenzi kwa muda usio pungua mwezi mmoja na usio zidi miezi mitatu. | 150/= kwa kila mita ya urefu |
| 3. | Ada ya kuweka uzio wakati wa ujenzi kwa muda usio pungua miezi mitatu na usio zidi miezi sita | 200/= kwa kila mita ya urefu |
| 4. | Ada ya kuweka uzio wakati wa ujenzi kwa muda usio pungua miezi sita na usio zidi miezi kumi na miwili | 400/= kwa kila mita ya urefu |

## SEHEMU YA KUMI NA TATU

## USHURU WA LESENI ZA ZABUNI

| **Namba** | **Aina ya kibali** | **Kiwango cha ushuru (Shilingi)** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa pombe za kienyeji | 12,000/= Kwa miezi sita |
| 2. | Ushuru wa pombe za kigeni | 30,000/= Kwa miezi sita |
| 3. | Maombi ya zabuni | 50,000 - 100,000/= Kwa zabuni moja |
| 4. | Leseni za biashara | 10,000/= - 500,000 Kwa mwaka ikizingatia na thamani pia na ukubwa wa biashara |

**SEHEMU YA KUMI NA NNE**

**ADA YA KUTUMIA JENGO AU KIBANDA, KIOSKI AU MEZA ZA HALMASHAURI**

| Namba | Aina ya chombo | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kibanda Sokoni | 50,000/=Kwa mwezi. |
| 2. | Kibanda Stendi | 80,000/=Kwa mwezi |
| 3. | Vizimba | 9,000/=Kwa mwezi. |
| 4 | Meza au kichanja | 500/=Kwa siku za soko |

**SEHEMU YA KUMI NA TANO**

**ADA YA KUPIMA AFYA KWA WAHUDUMU**

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kupima wahudumu kila mhudumu wa nyumba ya kulala wageni, hoteli, mgahawa, saluni, wafanyakazi wa viwanda vya kuzalisha vinywaji, wauzaji wa vyakula vilivyopikwa au kukaaangwa anawajibika kusajili kwa Halmashauri ili kubainisha ukamilifu wa afya yake kuendesha shughuli husika | 10,000/=Kwa mwaka. |

**SEHEMU YA KUMI NA SITA**

**USHURU WA MBAO ZA MATANGAZO**

| Namba | Aina ya matangazo | Kiwango cha ushuru | ukubwa | muda |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Matangazo yatakayoandikwa kwenye vibao na kuwekwa kando ya barabara<br>[yasiyotoa hai]<br>[yanayotoa hai] | 25,000/=<br>40,000/= | Kila futi mraba moja<br>Kila futi mraba moja | Kwa mwaka<br>Kwa mwaka |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | Matangazo ya biashara yatakayoandikwa na kubandikwa kwenye nyumba<br>[a] yasiyotoa mwanga<br>[b] yanayotoa mwanga<br>[c] Aina zote za matangazo ya kubandika ukutani na mengineyo | 80,000/=<br>120,000/=<br>15,000/= | Kila mita moja ya mraba<br>Kwa mita moja ya mraba | Kwa mwaka<br>Kwa mwaka |
| 3. | Matangazo ya biashara kwa njia ya kipaza sauti | 20,000/= | Kwa siku | Kwa siku |
| 4. | Kuweka kibao au tangazo(Kibali) | 5,000/= | | Kwa mwaka<br>Kwa mwaka |
| 5. | Minara kibali kwa ajili ya kusimika | 500,000/= | Kwa mnara mmoja | Kwa mwaka<br>Kwa mwaka |
| 6. | Minara ya mawasiliano katika maeneo yote ya Halmshauri | Kwa mujibu wa Mkataba | | Kwa mujibu wa Mkataba |

**SEHEMU YA KUMI NA SABA**

**ADA YA USAJILI WA TEKSI NA BAJAJI**

| **Namba** | **Aina ya chombo cha usafiri** | **Kiwango cha ada** | **muda** |
|---|---|---|---|
| 1. | Teksi | 60,000/= | Kwa mwaka |
| 2. | Bajaji | 60,000/= | Kwa mwaka |
| 3. | Pikipik | 30,000/= | Kwa mwaka |

**SEHEMU YA KUMI NA NANE**

**USHURU WA KUTUMIA STENDI**

| **Namba** | **Aina ya chombo cha usafiri** | **Kiwango cha ushuru (shilingi)** |
|---|---|---|

*Tangazo La Serikali Na. 459 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria 40 na kuendelea | 2,000/= |
| 2. | Basi la abiria kuanzia 21 mpaka 49 (coaster) | 1,500/= |
| 3. | Basi dogo (hiace, Noah na mengineyo) | 1,000/= |
| 4. | Teksi | 1,000/= |
| 5. | Gari binafsi | 500/= |
| 6. | Bajaji | 500/= |
| 7. | Pikipiki | 500/= |
| 8. | Magari madogo ya mizigo (pickup) | 1,500/= |
| 9. | Ada ya kutunza gari lililokamatwa au kuzuiliwa | 10,000/= |

## SEHEMU YA KUMI NA NANE

## USHURU WA MAEGESHO

| **Namba** | **Aina ya chombo cha usafiri** | **Kiwango cha ushuru** | **Muda** |
|---|---|---|---|
| 1. | Teksi | 500/= | Kwa siku |
| 2. | Pikipiki au bajaji | 300/= | Kwa siku |
| 3. | Magari ya abiria, mfano mabasi na coaster, | 1,500/= | Kwa siku |
| 4. | Hiace, landrover, noah na magari mengine madogo | 1,000/= | Kwa siku |
| 5. | Kulaza malori (tani 11-30) eneo lililotengwa na Halmashauri | 5,000/= | Kwa usikun mmoja |
| 6. | Kulaza malori kuanzia Kg 800- tani 10 Eneo lililotengwa na Halmashauri | 3,000/= | Kwa usiku mmoja |
| 7. | Kulaza magari mengine eneo lilitengwa na Halmashauri | 2,000/= | Kwa siku |

## SEHEMU YA KUMI NA TISA

## USHURU KATIKA MAGULIO NA MINADA YOTE

| **Namba** | **Aina ya mazao** | **Kiwango ushuru (shilling)** |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ulezi gunia | 1,000/= |
| 2. | Ndizi mbichi mkungu (mkao) | 200/= |
| 3. | Ndizi mbivu Debe au plastiki | 200/= |
| 4. | Nyanya – Tenga | 300/= |
| 5. | Nyanya – debe | 200/= |
| 6. | Kabeji-Gunia | 300/= |
| 7. | Mahindi-Gunia | 500/= |
| 8. | Vinywaji (juisi, barafu) sanduku ya kuwekea chupa za soda, kontena, kasha la barafu la kuhifadhi vinywaji. | 200/= |
| 9. | Mafuta ya kupikia ndoo au Debe | 200/= |
| 10. | Sabuni za kufulia au kuogea katoni. | 200/= |
| 11. | Majembe au mapanga | 500/= |
| 12. | Magadi-Gunia | 200/= |
| 13. | Samaki au dagaa | 200/= |
| 14. | Samaki tenga | 300/= |
| 15. | Mafuta ya taa kwa siku (mkao) | 500/= |
| 16. | Viatu,Raba,Malapa kwa siku (mkao) | 500/= |
| 17. | Matunda aina zote- Gunia | 200/= |
| 18. | Asali, Mafuta (mkao) | 3,000/= |
| 19. | Matunda – Lori | 2,000/= |
| 20. | Matunda – gari ndogo aina ya pick up | 2,000/= |
| 21. | Viazi,Karoti,Vitunguu, Njegere- Lori | 300/= |
| 22. | Viazi, Karoti, Vitunguu, Njegere- gari ndogo aina ya pick up | 1,000/= |
| 23. | Nazi – Gunia | 300/= |
| 24. | Udalali sokoni kwa siku. | 1,000/= |
| 25. | Mboga za Majani- Gunia | 200/= |
| 26. | Mtama, Ufuta – debe | 200/= |
| 27. | Tumbaku au Sonyo | 300/= |
| 28. | Bidhaa za madukani zilizopangwa sokoni. | 1,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 29. | Maharage – gunia | 1,000/= |
| 30. | Mchele – gunia | 1,000/= |
| 31. | Samaki wabichi – gari ndogo aina ya pick up. | 2,000/= |
| 32. | Mitumba robota | 500/= |
| 33. | Miwa (mkao) | 500/= |
| 34. | Kuku tenga | 1,000/= |
| 35. | Mbuzi, kondoo, nguruwe | 2,000/= |
| 36. | Bidhaa nyinginezo kwa mkao | 200/= |

**JEDWALI LA PILI**

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 23)*

**FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA**

Mimi …………………………………. nakiri **KWA HIARI YANGU MWENYEWE** mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Hai, kwamba mnamo tarehe ………… ya mwezi…………. Mwaka ……… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ……………cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya wilaya ya hai ya Mwaka, 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, Niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

**NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.**

Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………

Jina: ……………………………...
Saini: …………………………….
**MBELE YANGU:**
Jina: ……………………………………
Wadhifa: ……………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Hai imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika tarehe 12 mwezi Mei, mwaka .

DIONIS M. MNYINGA
*Mkugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Hai*

EDMUND RUTARAKA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Hai*

NAKUBALI,

L.S

Dodoma,
5 Disemba, 20243

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*